Mtazamo Dhidi Ya Mungu Sehem Ya 2 – Je Unaushirika Wa Ndani Na Mungu Aliyehai?

(Attitude Towards God Part 2 – Do You Have A deep Fellowship With The Living God?)

Na

Ellis P. Forsman

Mtazamo Dhidi Ya Mungu Sehem Ya 2 – Je Unaushirika Wa Ndani Na Mungu Aliyehai?

(Attitude Towards God Part 2 – Do You Have A deep Fellowship With The Living God?)

Na

Ellis P. Forsman

Okt. 6, 2011

Mtazamo Dhidi Ya Mungu Sehem Ya 2 – Je Una Ushirika Wa Ndani Na Mungu Aliyehai?

1 Yohana 1:

Mtazamo sahihi hakika ni muhimu.

Zaburi 100:2-4, "*Mtumikieni BWANA kwa furaha; njooni mbele zake kwa kuimba; jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni maalangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, lihimidini jina lake;*"

Mitazamo sahihi ni muhimu kwa ajili ya umoja katika kusanyiko la mahali fulani. Karama zote zilizo katika dunia haziwezi kutokea kwa mitazamo mibovu ambayo tunaweza kuwa nayo. Mit. 23:7, "*Maana aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo…*"

Kwa mtazamo sahihi, juhudi zetu katika kumtumikia Bwana wetu urithiwa na kuishi kikamilifu.

Mtazamo unatafsiriwa: Ni hali ya akili au hisia, kutokuwa sawa.

Kwa maneno mengine, ni hali ya mtu kutambua kitu.

Kidini tunaweza kuwa na mtazamo unaoleta baraka toka kwa Mungu, au ile isiyoleta upendeleo toka kwake.

Hebu na tuangalie baadhi ya mitazamo tunayopaswa kuwa nayo dhidi ya Mungu.

Tunapaswa kuwa na hakika wa kushikilia mtazamo mzuri katika maisha haya kama tunatarajia kupokea baraka zake. Moja ya vitu katika maisha haya ni ushirika wa karibu na Mungu.

Ushirika ni hitaji mhimu la mwanadamu. Pasipo hiyo watu huteseka. Pasipo hiyo, matadizo ya ziada hutengenezwa. Watu wengine hawafanyi vizuri wanapoachwa peke yao katika dunia.

Usafi binafsi unaachwa bila kutekelezwa.

Upweke na hofu mara nyingi huingia.

Rafiki yangu alijinyonga baada ya ndugu yake pekee aliyekuwa hai (kaka) kufariki. Alikuwa amekandamizwa na mpweke, hivyo akaamua kuutoa uhai wake mwenyewe.

Maisha hufurahisha zaidi tukiyashiriki na wale tunaowapenda.

Gazeti la Uingereza lilitoa zawadi ya pesa kwa jibu bora juu ya swali, "Ni njia gani ya mkato inayoweza kumfikisha mtu London?" Jibu lililoshinda zawadi hiyo ya fedha ni, "Njia ya mkato inayoweza kumfikisha mtu London ni ushirika mzuri."

Wasafiri wote wanafahamu ukweli kiasi gani jinsi jibu hilo lilivyo. Ushirika mzuri unafupisha safari yetu, haijalishi ni umbali gani.

Katika ushirika kama huo wakati unapaa, umbali unateleza kwa haraka, na mwisho unafikiwa kabla mtu hajaigundua.

Njia ya kwenda mbinguni imefupishwa sana; barabara imefanywa rahisi, wakati Yesu Krissto ndiye mshirika wetu wa safari.

Ushirika mkuu duniani ni ushirika na Mungu; lakini kwa watu wengi, ushirika huu umeachwa kwa sababu ya dhambi zao.

Isa. 59:1-2, "*Tazama mkono wa BWANA haukupunguka, hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia.*"

Kila mmoja anahitaji ushirika huu urejeshwe. Rum. 3:23, "*Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*" Rum. 6:23, "*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*"

Kama ushirika huu ukiachwa usimame katika hali kama hii, majibu ya mwisho ni umilele katika nchi ya jehanam.

Ushirika wa kindani na Mungu ni muhim katika kupata uzima wa milele.

Tuna shirikiana na wakina nani?

Katika kipeperushi hiki tunataka kujifunza ukweli kuhusu ushirika wa kindani na Mungu aliye hai.

Ushirika na Baba.

1 Yohana 1:3, "*Hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi piampate kushirikiana nasi: na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo.*"

Mungu ni mmumba wetu, Mtetezi, Baba, Msaidizi, Mlinzi, Mwenye nguvu na Mwalimu. Hakuna moja katika sifa hizi ambayo tunaweza kujaribu kuzikosa. Ni lazima tuudhamini urafiki huo, la sivyo tutajikuta katika hali mbaya.

Ufu. 3:4, "*Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili.*"

Wachache katika Sardi waliwezaa kuonja ushirika wa kindani na Mungu. Kwa nini? Kwa sababu waliyatunza mavazi yao meupe – hawakuishi maisha ya dhambi.

Ushirika na Mwana.

- 1 Kor. 1:9, "*Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwingie katika ushirika wa Mwanaye, Yesu Kristo Bwana wetu.*"
- Mat. 18:20, "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.*"
- Yohana 12:26, "*Mtu akinitumikia na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu.*"
- Yohana 15:15, "*Siwaiti tena watumwa, kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu.*"

Yesu aliishi maisha kamilifu pasipo na dhambi kama mfano wetu; alikufa kifo kibaya msalabani kwa ajili ya dhaambi zetu; alinunua miili yetu kwa damu yake; akaanzisha kanisa mahali ambapo ndugu wanaweza kuja pamoja na kukumbuka dhabihu yake na kumjia kila mmoja nguvu; na sasa anajenga mji wa milele kwa marafiki zake wapendwa. Katika Siku ya Hukumu na atawawakilisha watakatifu. Hatuna rafiki mkuu kuliko Yesu. Je tunaweza kuendelea pasipokuwa na urafiki wake?

Ushirika wa kindani na Mungu ni nini?

Nini ambacho siyo.

Siyo jamaa wa kawaida – watu wengi wanadai "kumfahamu Mungu", lakini wanashindwa kuonyesha kawaida hiyo iliyopo katika maisha yao.

Katika mfumo huo naweza kudai kwamba namfahamu T. A. Wilson, mwenyekiti aliyepita wa Kampuni ya Boeing, na sasa anaugua; na Albert Rossellini, gavana aliyepita wa mji wa Washington; wote niliowahi kuongea nao. Ushirika wa ndani unahitaji mazungumzo ya kila siku.

Ushirika wa ndani na Mungu siyo ile inayotegemeana na hali yako.

Nilipofanya kazi upande wa Upepo miaka iliyopita, nilikuwa na uhusiano mzuri na mkuu wangu, Jeff. Tulikuwa marafiki, lakini alikuwa

na mamlaka. Niliiheshimu na sikuibadilisha. Aliponipa mwongozo, niliifuata kulingana na alivyotaka ifanyike, siyo nilivyofikiri ingefanyika. Wakati Jeff alipokuwa ametoka, wakati mwingine alikuwa anamweka Marko katika uongozi na wakati mwingi alikuwa ananiweka mimi pia katika uongozi. Kila mmoja wetu aliyepewa mamlaka ya uongozi alifanya kulingana na jinsi tulivyoagizwa kufanya. Unadhani ingetokea nini kama ningemwambia Jeff (au Marko kama angekuwa kwenye madaraka), "Sitafanya hicho!"? ningejikuta naumiza uhusiano wetu, kupewa adhabu, na ikiwezekana kufukuzwa kwa sababu ya mytazamo wangu wa kuchukulia kirahisi mamlaka yao.

Watu wengi leo hawaelewi kwamba wanaumiza uhusiano wao na Mungu na wanauzika mamlaka yake pale wanapokataa mwongozo wake. Wanafanya hivyo pale wanapotoa kauli kama, "Sidhani kama ubatizo ni muhim", au "Kanisa lolote litafanya", au "wanafurahisha" badala ya kulihubiri neno la Mungu.

Rum. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Ushirika wa ndani na Mungu ni zaidi ya uhusiano wa dharura (kama sehemu ya huduma ya kwanza). Kwa watu wengine inasababisha hali ya kutishiwwa maisha kabla hawajafikiri kuhusu Mungu.

Ushirika wa ndani Mungu ni.

Kujitoa kwa asilimia zote. Mat. 16:24, "*Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate.*"

Kuubeba msalaba siyo kuvumilia mambo kama umasikini, ugonjwa, hali mbaya na hewa, au kitu kingine kinacho sababisha kutotulia, bali ni mizigo iliyokubaliwa ya maisha kwa sababu ya mapenzi ya Mungu. Wakati ikiwa ni kweli Mkristo anajikana mwenyewe kwa starehe nyingi katika maisha haya, kubeba msalaba unamanisha kuvumilia dhihaka na matusi yaw engine unaposimama kwa ajili ya Mungu katika maisha yetu.

Ushirika wa ndani na Mungu ni ile inayotegemea hali yake.

Yohana 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba , ila kwa njia ya mimi.*"

Watu wanapenda kusikia Yohana 15:16 na kuwaambia wengine kuhusu maneno yake. Yohana 15:16, "*Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi, nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa jina langu awape.*"

Wanasisitiza "*chochote*" tunachoomba tutakipata, lakini wanakataa nyingine "*chochote*" mistari miwili katika kuelekea katika hii:

Yohana 15:14, "*Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamruyo.*"

Upendo wa Mungu ni wa masharti. Yeye ndiye aliyeliweka neno "*kama*" katika uhusiano wetu. Tusipokuwa marafiki zake wa kweli ushirika wetu hautakubaliwa.

Nilimsikia mwinjilisti wa redioni akidai kwamba Kristo hakufanya upendo wake kuwa wa masharti. Hajui anachokiongelea.

- Yohana 15:14, "*Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamruyo.*"
- Yohana 14:15, "*Mkinipenda mtazishika amri zangu.*"

Ushirika wa ndani na Mungu unaanzia kwenye upendo.

1 Yohana 4:19, "*Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza.*"

Yesu ameonyesha upendo wake kwetu kwa kuutoa uhai wake msalabani. Yohana 15:13, "*Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.*"

Marafiki zake pia wanatoa upendo wao kwake. Efe. 6:24, "*Neema na iwe pamoja na wote wampendao Bwana wetu Yesu Kristo katika hali ya kutokuharibika.*"

Upendo huo lazima uwe upendo wa kweli – ile isiyopotea tunapojisikia kwamba Yesu ahitajiki; upendo ambao ni mwingi wakati amabo ni mzuri na wakati ambao ni mbaya. Tunapomwonyesha kwamba tunampenda, atakaa pamoja nasi. 1 Yohana 4:16, "*Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake.*"

Kwa njia nyingine (kinyume): Kama ukikataa kukaa ndani ya Mungu, usitarajie kwamba atakaa ndani yako, kwa sababu hawezi.

Jinsi wengine wanavyowajibika

Wengine wanawajibika nusu-roho.

Kama mke wa Lutu. Alijiingiza katika majaribu kuangalia nyuma kwa marafiki zake na ndugu waliobaki nyuma wakati Mungu alipoangamiza miji ya Sodoma, baada ya Mungu kusema wasiangalie nyuma. Luka 17:31-32, "*Katika siku ile aliye juu ya dari, na vyombo vyake vimo ndani ya nyumba asishuke ili kuvitwaa; na kadhalika aliye shambani asirejee nyuma. Mkumbukeni mkewe Lutu.*"

Tunapofanya huduma ya Mungu katika maisha yetu, hatupaswi kuangalia nyuma kwa kutamani maisha yetu ya awali. Mtazamo wetu pale tunapofanyika Wakristo ni kuwa kwa Yesu Kristo na huduma yetu kwake.

2 Pet. 2:20-22, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli. Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*"

Hatupaswi kumhudumia nusu-roho.

Wengine wamewajibika kwa kukalifu.

Watu wengi ni wakalifu katika huduma yao kwa Mungu. Wametingwa na kujali maisha haya.

Luka 8:11-14, "*Na huo mfano maana yake ni hii; mbegu ni neno la Mungu. Wale wa karibu na njia ndio wasikiao, kisha huja Ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka. Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga. Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote.*"

Tunaporuhusu kujali kwa maisha haya yaingie katika maisha yetu upendo wetu kwwa Yesu hautakuwa na nguvu ya kutosha kuweza kutukidhi. Tukimweka kuwa wa kwanza katika maisha yetu, atashughulikia mahitaji yetu.

Hii inajumuisha kazi zetu, shule, michezo, nk. Ambazo tunaruhusu ziingilie uhusiano wetu na yeye.

Wengine wanawajibika katika udhuru.

Watu wengine wanaweka udhuru. Luka 14:16-24, "*Akawaambia mtu mmoja alifanya karamu kubwa akaalika watu wengi, akamtuma mtumwa wake saa ya chakula awaambie wale walioalikwa, Njooni kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari. Wakaanza wote kutoa udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, nimenunuaa shamba sharti niende nikalitazame; tafadhali unisamehe. Mwingine akasema nimenunua ng'ombe jozi tano, ninakwenda kuwajaribu, tafadhali unisamehe. Mwingine akasema nimeoa mke, na kwa sababu hiyo siwezi kuja. Yule mtumwa akaenda akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, toka upesi uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete. Mtumwa akasema Bwana hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi. Bwana akamwambia mtumwa, toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa. Maana nawaambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu.*"

Ushirika na Mungu unahitaji kuwajibika kikamilifu, siyo yule anayetafuta udhuru.

Ushirika wa ndani na Mungu unaanzaje?

Katika kutambua dhambi. Tunapaswa kutambua kwamba tunapotenda dhambi ushirika wetu na Mungu unahatarishwa. Tunapotambua kwamba hali hii imetokea, tunapaswa kutubu na kutii injili.

Tunapoyakimbia machafu ya dunia, tunaweza kuwa washirika wa upendo wa Mungu na ahadi.

Wengine wanadhani kuwa dhambi zao zimekuwa nzuri kiasi kwamba hawawezi kufikiria kuwa Wakristo. Paulo ni mfano wa mtu aliyekuwa wakati mbaya, lakini alibadilika. Petro alimkana Kristo, lakini alitubu. Kumbuka, kila mmoja ametenda dhambi. Hauko pekee yako.

2 Pet. 1:4, "*Tena kwa hayo ametukirimia ahadi ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*"

Hataivyo, dhambi ni lazima ife kaatika maisha yetu ili kufurahia ushirika wa ndani na Mungu. Rum. 6:1-6, "*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja*

naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."

Kama tukikataa dhambi katika maisha yetu na kuukubali ushirika wa Yesu, maisha yetu yatatajirika zaidi kwalo.

Miongoni mwa Wadachi mauwa yalikuwa yakilimwa kwa kupandwa uwa lililoshindwa karibu na ua lililofanya vizuri. Ua hili lilifanya vizuri lilikuwa likiangaliwa kwa makini, na sehemu ya juu ili kuepuka kujizalisha yenyewe; tendo ni kwamba iweze kusaidiwa na ua lilikuwa likifanya vizuri.

Hii ndo njia ambayo maisha yetu yanapaswa kuwa pamoja na ile ya Yesu. Kama maisha yetu yakitapanywa, kama ilivyokuwa, kwa haki yake katika mioyo yetu, basi itapoteza ubora wa uzuri wake, na kuhamishwa katika ubora zaidi wa Kristo.

Maisha yetu lazima yawe na kutembea kwa imani. 1 Yohana 1:6-7, "*Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo wala hatuifanyi iliyo kweli; bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*"

Ni matokeo yapi yaliyopo katika kuwa na ushirika wa ndani na Mungu?

Ushirika. Na Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu. (angalia 1 Yohana 1:6-7 hapo juu). Pia tuna ushirika sisi kwa sisi. (angalia 1 Yohana 1:6-7 hapo juu.)

Matokeo ya ushirika wa ndani na Mungu inajionyesha katika maisha yetu na matendo. Tunaonyesha upendo, uvumilivu, furaha, amani, furaha, nk.katika maisha yetu.

Pia tunaushirika wa ndani na injili. Fil. 1:3-5, "*Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, siku zote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi.*"

Tukimpenda Mungu hakika, matamanio yetu pia ni kukaa katika neno alilotupatia.

Wakati fulani nilisoma yafuatayo kuhusu binti mmoja na tabia zake za kusoma:

Msichana wakati fulani aliweka kitabu chini ambayo alimaliza kusoma, na kauli kwamba ni kitabu kibaya ambacho hajawahi kusoma.

Kwa sababu ya muda, akachumbiwa na mwanamume; na usiku mmoja akamwambia, "Nina kitabu katika maktaba yangu ambayo jina la mwandishi na pia jina la kwanza, zinafanana na yako. Je hii siyo jambo geni?"

"Sidhani", kijana alijibu.

"Kwa nini?", binti aalisema.

"Sababu rahisi, kwamba niliandika kitabu."

Usiku huo binti huyo alikaa hadi saa 2 asubuhi akisoma kitabu tena. Na wakati huu ilionekana kama kitabu kinachomvutia ambacho hajawahi kukisoma.

Kitabu ambacho kilikuwa kibaya sasa ni kizuri kwa sababu alimfahamu na kumpenda mwandishi.

Hivyo, mwana wa Mungu anapata Biblia inamvutia kwa sababu anamfaham na kumjua mwandishi!

Tukidhani kuwa Biblia ni mbaya, ni wakati wa kuangalia mtazamo wetu na uhusiano na Mungu.

Hitimisho

Vipi kuhusu wewe? Mtazamo wako ni upi dhidi ya Mungu? Je uko katika ushirika na Mungu?

Ushirika huo ni wa ndani kiasi gani?

Kama kuna kitu katika maisha yako ambayo inasababisha bonde katika uhusiano huo na Mungu, kwa nini usifanye jambo kulihusu leo?

Usiwe kama Felix, aliyemwambia Paulo, "*Nenda kwa wakati huu; nikiwa na wakati muafaka, nitakuita.*" Hakuna ishara kwamba "wakati mwafaka" ulimwijia.

Zifuatazo ni hatua muhim kwa uhusiano wa ndani na Mungu; mtu lazima kwanza awe Mkristo:

- **Imani.** Waeb.11:6, "*Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna

Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend 11:18, *"...Mungu amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani!" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "*Katika*" inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi

gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "imekuwa kwetu **sisi** "*kuitimiza haki yote*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya ubatizo? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*" Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile "*Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.*" (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kaburini kwa kuweka udongo mdogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa Mkristo, kwa nini usizingatie leo?